

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA**



TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

18/09/2026 DODOMA

Wizara ya Viwanda na Biashara inapenda kuwaalika wananchi wote kwenye mnada wa hadhara wa vifaaa chakavu. Lengo la mnada huo ni kuuza vifaa chakavu vya Tehama, vifaa na Samani za ofisi. Mnada huo utafanyika katika Makao Makuu ya Wizara Mji wa Serikali Mtumba - Dodoma kama ilivyooneshwa katika jedwali lifuatalo.

TAREHE YA MNADA	KITUO/SEHEMU MALI ILIPO	AINA YA MALI ZITAKAZOUZWA
26/09/2026 Siku ya Jumamosi	Mji wa Serikali Mtumba - Dodoma	1) Vifaa vya Tehama; 2) Vifaa vya ofisi; 3) Samani za ofisi.

Masharti ya mnada

- Mnada utaanza saa nne (4:00) asubuhi.
- Mali zote zitauzwa kama zilivyo.
- Mnunuzi atakiwa kulipa asilimia mia moja (100) ya bei ya kifaa atakachonunua papo hapo siku ya mnada.
- Mnunuzi atatakiwa kuhamisha kifaa atakachonunua ndani ya siku ya mnada.
- Ruhusa ya kuangalia mali itatolewa siku moja (1) kabla ya tarehe ya mnada.

NYOTE MNAKARIBISHWA

IMETOLEWA NA KATIBU MKUU, WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA